UBAINIFU KUHUSU

i. MAFUNGU YA WATU KATIKA SAUMU YA RAMADHANI

ii. MAMBO YENYE KUFUNGUZA NA MASHARTI YAKE

Mwandishi

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud

Pongwe Tanga

Tanzania

Simu: 0715263253.

Hii ni Makala yetu ya pili katika kuikumbusha nafsi yangu na ndugu zangu waislamu hukumu mbalimbali za kisheria katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani ili tuitekeleze ibada hii ipasavyo na iwe sababu ya kupata rehma za Allaah na radhi zake.

Ninasema: Watu katika ibada ya funga wamegawanyika katika mafungu kumi:

Fungu la kwanza: Muislamu, Baleghe, Mwenye akili, Mkazi (si msafiri), Muweza, na Amesalimika na vizuizi:

Mtu yeyote aliye kamilisha masharti hayo ni wajibu juu yake kufunga mwezi wa Ramadhani katika muda wake kwa ushahidi kutoka ndani ya Qur'an, Sunnah na Makubaliano ya waislamu juu ya hilo.

﴿شَهۡرُ رَمَضَانَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ فِيهِ ٱلۡقُرۡءَانُ هُدٗى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَٰتٖ مِّنَ ٱلۡهُدَىٰ وَٱلۡفُرۡقَانِۚ فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ ٱلشَّهۡرَ فَلۡيَصُمۡهُۖ﴾

"Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'an hali ya kuwa ni uwongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi ** Basi atakaye kuwa mjini (mkazi) katika mwezi huu naafunge[1]".

Na Mtume swala na salamu zimshukie amesema:

«إِذَا رَأَيْتُمُ الهِلاَلَ فَصُوْمُوا»

"Mtakapo Uona mwezi fungeni[2]".

Na wamekubaliana waislamu wote juu ya uwajibu wa kufunga mwezi wa Ramadhani kwa mtu aliye timiza masharti tuliyotaja.

---

[1]- Surat Al-Baqara/185.

[2]- Bukhari (1906) na Muslim (1081).

Ama kafiri haifai kwake kufunga na wala haisihi (haikubaliki) funga yake, kwa sababu yeye si katika wanaostahiki kufunga.

Na endapo akisilimu ndani ya mwezi wa Ramadhani si lazima kwake kufunga masiku yaliyo kwisha pita, kwa kauli ya Allaah:

﴿قُل لِّلَّذِينَ كَفَرُوٓاْ إِن يَنتَهُواْ يُغۡفَرۡ لَهُم مَّا قَدۡ سَلَفَ﴾

"Waambie wale walio kufuru: Wakikoma watasamehewa yaliyo kwisha pita[3]".

Na akisilimu katika mchana wa Ramadhani kutamlazimu yeye kujizuia masaa (muda) uliobaki wa siku hiyo kwa sababu amekuwa ni miongoni mwa wanaostahiki ndani wa wakati wa kufunga.

Fungu la pili: Mtoto mdogo:

Ama mtoto mdogo haipasi kwake yeye kufunga mpaka afikie Baleghe, kwa kauli ya Mtume swala na salamu zimshukie:

«رُفِعَ الْقَلَمُ عَنْ ثَلَاثٍ: عَنِ النَّائِمِ حَتَّى يَسْتَيْقِظَ، وَعَنِ الصَّبِيِّ حَتَّى يَحْتَلِمَ، وَعَنِ الْمَجْنُونِ حَتَّى يَعْقِلَ»

"Imenyanyuliwa kalamu kwa (watu) aina tatu: kwa Mwenye kulala mpaka atakapo Amka, Mtoto mdogo mpaka atakapo Ota ndoto (ya jimai), na Mwenda wazimu (kichaa) mpaka atakapopata akili[4]".

Lakini ni wajinu mzazi au mlezi kumuamrisha yeye kufunga kwa ajili ya kumzowesha ili iwe ni wepesi kwake wakati atakapofika utu uzima, na huo ndiyo mwenendo wa watu wema walio tangulia, walikuwa wanawaamrisha watoto kufunga kisha wanaenda nao misikitini, mmoja wao akilia kwa sababu ya njaa

[3]- Surat Al-Anfaal/ 38.

[4]- Ahmad (Jz. 2, hadithi ya 1327). Abu Daud (4399) na wengine.

wanampatia vitu cha kuchezea ili apumbazike, tafauti na wazazi wengi hivi leo wameghafilika na jambo hili na baadhi yao huwakata watoto wao wasifunge kwa hoja ya kuwahurumia hali ya kuwa si sahihi, ndiyo, akifunga ukaona kwamba anapata madhara hakuna vibaya kumpatia chakula lakini ni vizuri kumzowesha akiwa mdogo.

- **Alama za baleghe kwa mtoto wa kiume:**
  1. Kuteremsha manii kwa kuota ndoto au sababu nyingine.
  2. Kuota nywele kwenye kinena pembezoni mwa tupu ya mbele
  3. Kutimiza miaka kumi na tano.

Ama kwa mwanamke kuna ziada ya alama nayo ni:

4. Kupata Hedhi.

Mwanamke akifika baleghe halafu akaanza kupata Hedhi katika mchana wa Ramadhani hali ya kuwa amefunga akamilishe funga yake na hakuna chochote juu yake, lakini akiwa hajafunga ajizuie muda uliobaki wa siku hiyo kwa sababu ni katika wanaostahiki kufunga na wala hatolipa kwa sababu yeye hakuwa miongoni mwa wanaostahiki tangu mwanzo wa kufunga (wakati wa alfajri).

Fungu la tatu: Mwenda wazimu:

Tumetangulia kutaja hadithi kuhusu watu wa aina tatu ambao haiandiki kwao kalamu jambo lolote katika mema au uovu, miongoni mwao ni Mwenda wazimu (kichaa/chizi): **“na Mwenda wazimu (kichaa) mpaka atakapopata akili”.** Kwa hiyo haisihi kwake funga kwa sababu hana akili ya kuweza kuzingatia ibada wala kunuwia, na ibada zote huzingatiwa Nia.

Lakini akiwa anapatwa na wazimu baadhi ya wakati na muda mwingine anazinduka (anapata akili) basi itamlazimu yeye kufunga wakati wa kuzinduka kwake na si wakati ule alipopata wazimu, na endapo asubuhi amenuwia kufunga halafu akapatwa na wazimu katika mchana wa Ramadhani funga yake ni sahihi ni sawa na mtu aliyezimia mchana wa Ramadhani kwa ajili ya maradhi au sababu nyingine, kwa sababu alitia Nia ya kufunga hali ya kuwa ana akili timamu na hakuna dalili yoyote ya kubatilisha funga yake hasa akijulikana kwamba unamtokea yeye wazimu katika baadhi ya muda na muda mwingine anakuwa mzima.

Na kwa kufanyia kazi kanuni hii hatolipa masiku ambayo alikuwa amepatwa (aliugua) ndani yake wazimu.

Na endapo Mwenda wazimu zimerejea kwake akili katika mchana wa mwezi wa Ramadhani itamlazimu ajizuie muda uliobaki wa siku hiyo kwa sababu amekuwa ni miongoni mwa wanao wajibika kufunga na wala hatolipa siku hiyo, ni sawa na mtoto akipata Baleghe au kafiri akisilimu katika mchana wa Ramadhani.

Fungu la nne: Mtu mzima ambaye hawezi kupambanua:

Mtu huyu hana uwajibu wa kufunga wala kulisha masikini kwa sababu imeondoka kwake takliif (kulazimishwa na sheria) kwa hiyo ni kama mtoto mdogo ambaye hawezi kupambanua kitu. Na akiwa anaweza kupambanua baadhi ya wakati basi ni wajibu wake kufunga wakati wa kujitambua kwake si wakati wa kuchanganyikiwa, na swala pia ni kama funga itamlazimu kuswali wakati anapopata fahamu.

Fungu la tano: Mwenye kushindwa kufunga kabisa:

Mfano wake ni mgonjwa ambaye hakuna kwake matarajio ya kupona kama vile mgonjwa wa Saratani (Cancer) n.k, au mtu mzima ambaye ni tabu kwake kufunga hao si wajibu kwao kufunga kwa sababu ya kushindwa na badala yake atalisha masikini mmoja kila siku ambayo atashindwa kufunga.

- **Namna ya kulisha masikini:**

Mtu amepewa hiyari ima kutoa kila siku kwa kumpa masikini fidia ya chakula kinacho pendwa sana katika mji au atapika chakula na kuwatosha masikini kwa idadi ya siku ambazo hakufunga na fidia ni nusu ya pishi ya Mtume swala na salamu zimfikie ambayo ni sawa na kilo moja na robo, kwa sababu pishi ya Mtume swala na salamu zimfikie kwa vipimo vya kisasa ni sawa na kilo mbili na nusu kwa sanadi sahihi kutoka kwa swahaba Zaid Bin Thabit Allaah amridhie na hilo wametusimulia baadhi ya masheikh.

Fungu la sita: Msafiri ambaye hajakusudia kukimbia kufunga:

Kama mtu amesafiri ili aache kuacha kufunga basi jambo hilo kwake ni haramu na ni wajibu kwake kufunga. Na kama hajakusudia hilo basi amepewa hiyari baina ya kufunga au kula akiwa safarini na atalipa katika masiku mengine, ni sawa umerefuka muda wa safari yake au umekuwa mfupi kama vile dereva wa ndege (pilot) au basi za abiria kwa kauli ya Allaah:

﴿وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ۚ يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ﴾

"Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini basi atimize hesabu katika siku nyingine. Allaah anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito[5]".

[5]- Surat Al-Baqara/185.

Na kauli ya Anas Bin Malik Allaah amridhie:

«كُنَّا نُسَافِرُ مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَلَمْ يَعِبِ الصَّائِمُ عَلَى المُفْطِرِ، وَلاَ المُفْطِرُ عَلَى الصَّائِمِ»

"Tulikuwa tunasafiri pamoja na Mtume swala na salamu zimshukie wala hakumlaumu aliyefunga juu ya aliyekula, wala aliyekula juu ya aliyefunga[6]".

Ndiyo maana Abu Said Al-Khudriy akasema:

«يَرَوْنَ أَنَّ مَنْ وَجَدَ قُوَّةً فَصَامَ، فَإِنَّ ذَلِكَ حَسَنٌ وَيَرَوْنَ أَنَّ مَنْ وَجَدَ ضَعْفًا، فَأَفْطَرَ فَإِنَّ ذَلِكَ حَسَنٌ»

"(Walikuwa Maswahaba) wanaona yule anayepata nguvu na akafunga basi (kufanya) hivyo ni vizuri na anayepatwa na kuchoka akala (pia) hivyo ni vizuri[7]".

Endapo dereva hawezi kufunga anapokuwa safarini kwa sababu ya joto kali au kuchoka basi ameruhusiwa kula na atakuja kukamilisha idadi ya siku alizoacha katika siku nyingine.

Na iliyo kuwa bora kwa msafiri afanye lile lenye wepesi kwake, lakini kama hapati tabu iliyo bora zaidi kwake ni kufunga ili afanye haraka kutekeleza wajibu wake na kuondosha dhima.

Na endapo msafiri ameingia katika mji wake mchana wa Ramadhani hali ya kuwa hakutia Nia ya kufunga wakati alipokuwa safarini haitafaa kwake kufunga kwa sababu Nia ya funga ya Ramadhani ni kabla ya kuchomoza alfajiri, kwa hiyo ataendelea kula mchana wa siku hiyo wala hatajizuia isipokuwa afanye hilo kwa siri na atakuja kulipa siku hiyo baada ya Ramadhani.

---

[6]- Bukhari (1947) na Muslim (1116).
[7]- Muslim (1116).

Fungu la saba: Mgonjwa mwenye matarajio ya kupona:

Mgonjwa wa aina ana hali tatu:

Hali ya kwanza: Ni kuwa hapati tabu yoyote endapo atafunga, katika hali hii ni wajibu wake kufunga kwa sababu hana udhuru.

Hali ya pili: Ni kuwa kufunga ni dhiki kwake hata kama hapati madhara, katika hali hii atakula na atakuja kulipa akipona.

Hali ya tatu: Ni kuwa kufunga kunamletea yeye madhara, hapo ni wajibu wake kula na haifai kwake kufunga, kwa sababu sheria imekataza mtu kuidhuru nafsi yake.

Allaah anasema:

﴿وَلَا تَقْتُلُوا أَنفُسَكُمْ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا﴾

"Wala msijiue, hakika Allaah ni Mwenye kuwahurumieni[8]".

Kwa maana msifanye jambo la madhara ambalo litakuwa ni sababu ya kujiangamiza au kumuangamiza ndugu yako muislamu.

Na Mtume swala na salamu zimshukie amesema:

«وَلِنَفْسِكَ عَلَيْكَ حَقًّا»

"Na nafsi yako ina haki juu yako[9]".

Na miongoni mwa haki zake ni kwamba usiitie kwenye madhara ukafunga huku unapata madhara hali ya kuwa kuna ruhusa kutoka kwa Allaah ya kula kisha uje kulipa ukipona.

---

[8]- Surat An-Nisaa/29.

[9]- Bukhari (1968).

Na akipatwa na maradhi katika mchana wa ramadhani hali ya kuwa amefunga na akashindwa kuendelea na saumu yake itafaa kwake kufungua (kula) kwa ile ruhusa aliyopewa na sheria.

Lakini kama alikuwa mgonjwa halafu akapona katika mchana wa Ramadhani hali ya kuwa hakufunga (amekula asubuhi) haifai kwake kufunga siku hiyo kwa sababu funga ya Ramadhani inaanza wakati wa asubuhi na wala hatajizuia na kula bali atakuja kulipa.

Na kama Daktari (Doctor) amethibitisha kwamba funga itampelekea yeye kudhurika au kuchelewa kupona itafaa kwake kula katika mchana wa Ramadhani kwa ajili ya kulinda afya yake na kujichunga na madhara, kama maradhi hayo ni yale yanayo tarajiwa kupona basi akipona atalipa siku alizoacha kufunga na kama haitarajiwi kwake kupona atakula na atatoa fidia kama ilivyotangulia.

Fungu la Nane: Mwanamke mwenye Hedhi:

Ni haramu kwake kufunga na wala haisihi saumu yake, kwa kauli yake Mtume swala na salamu zimshukie wakati akibainisha upungufu wa dini kwa mwanamke akasema:

«أَلَيْسَ إِذَا حَاضَتْ لَمْ تُصَلِّ وَلَمْ تَصُمْ»

"Je hakuwa anapopata Hedhi haswali wala hafungi?[10]".

Mwanamke akipata Hedhi mchana wa Ramadhani hali ya kuwa amefunga hata kama ni kabla ya kuzama jua kwa muda mchache funga yake imebatilika na atakuja kulipa isipokuwa ikiwa ni funga ya sunna hakuna juu yake wajibu wa kulipa.

[10]- Bukhari (304) na Muslim (79).

Na akitwaharika katika mchana wa Ramadhani haitafaa kwake kufunga siku hiyo kwa muda uliobaki, ataendelea kula katika mchana huo na wala hatajizuia.

Na akitwaharika usiku katika mwezi wa Ramadhani hata kama ni muda mchache kabla ya kuingia alfajiri ni wajibu juu yake kufunga kwa sababu hana tena kizuizi hata kama atachelewa kuoga (kujitwaharisha) mpaka asubuhi basi hakuna neno funga yake ni sahihi. Na mwanamke mwenye Nifasi hukumu zake ni kama mwanamke mwenye Hedhi.

Na ni wajibu kwa mwenye Hedhi au Nifasi kulipa funga tu tafauti na swala, kwa kauli ya Aisha Allaah amridhie wakati alipoulizwa kwa nini mwenye Hedhi analipa Funga lakini halipi Swala?

Akajibu:

«كَانَ يُصِيبُنَا ذَلِكَ، فَنُؤْمَرُ بِقَضَاءِ الصَّوْمِ، وَلَا نُؤْمَرُ بِقَضَاءِ الصَّلَاةِ»

"Ilikuwa inatupata sisi hiyo (Hedhi), tukawa tunaamrishwa kulipa funga wala hatuamrishwi kulipa swala[11]".

Fungu la Tisa: Mwanamke mwenye mimba au anayenyonyesha akihofia juu ya nafsi yake au mwanawe:

Endapo ana hofu kwamba akifunga atachoka au mwanawe atakosa maziwa ameruhusiwa kula katika mchana wa Ramadhani na atakuja kulipa siku zote alizoacha wakati akipata wepesi wa kufanya hivyo na pia kuna kauli nyingine kinyume na hii ya kwamba atakula na atatoa fidia ya kulisha masikini wala hatolipa, lakini asifanye hilo kwa makusudi kwa ajili ya kukimbia kufunga.

[11]- Mukhtasar ya sahihil Bukhari (403) na Muslim (335).

Fungu la Kumi: Mwenye kufungua ili kuzuia madhara kwa mtu mwingine:

Kama vile kumuokoa mtu anayezama baharini au mwenye kuteketea kwa moto na mfano wa watu hao, kama mwokoaji atahitajia kula au kunywa atafanya hivyo na atakuja kulipa siku hiyo. Na mfano wake ni mtu mwenye kuhitajia hilo kwa ajili ya kupambana na adui (Jihad) ni sawa akiwa safarini au katika mji wake atakula mchana wa Ramadhani na atakuja kulipa siku hiyo.

- Na endapo mtu baada ya kumalizika Ramadhani hakupona wala hakuweza kufunga mpaka akafa hakuna kitu juu yake.
- Lakini akipona kisha akazembea kwenye kulipa mpaka akafariki watafunga kwa niaba yake jamaa zake.
- Na kama hana ndugu wa karibu au wapo lakini hawataki kufunga basi watoe fidia kwa kulisha masikini.
- Na akichelewesha kulipa bila udhuru wa kisheria mpaka ikafika Ramadhani nyingine, ikimalizika atalipa siku alizoacha katika Ramadhani iliyotangulia na kuna kauli inasema: Atalipa pamoja na kutoa fidia kwa idadi ya siku alizoacha kwa sababu ya uzembe.

Ndugu msomaji haya ndiyo mafungu kumi ya watu katika saumu ya Ramadhani, angalia ni fungu gani unahusika nalo ili ufahamu hukumu zilizo katika fungu hilo.

Hii ni juhudi ndogo Allaah amenijaalia kuitoa na kuisambaza kwa ndugu zangu waislamu, bila shaka haiepukani na makosa katika uandishi au katika ufafanuzi wangu, mwenye kudiriki hilo anitaarifu kupitia namba yangu ya simu na mimi niko tayari kutengeneza pale nilipokosea. Wabillaahi Ttaufiiq

MAMBO 7 YENYE KUFUNGUZA (KUBATILISHA SAUMU):

Allaah anasema:

﴿وَكُلُوا۟ وَٱشْرَبُوا۟ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكُمُ ٱلْخَيْطُ ٱلْأَبْيَضُ مِنَ ٱلْخَيْطِ ٱلْأَسْوَدِ مِنَ ٱلْفَجْرِ ۖ ثُمَّ أَتِمُّوا۟ ٱلصِّيَامَ إِلَى ٱلَّيْلِ﴾

"Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku. Kisha timizeni Saumu mpaka usiku (kuzama kwa jua)[12]".

Katika aya hii tukufu Allaah Ta'alaa ametaja mambo makubwa yenye kufunguza na Mtume swala na salamu zimshukie akatimiza kwa kuyataja mengine kama ilivyothibiti katika hadithi.

Jambo la Kwanza: Kufanya Jimai (mchana wa Ramadhani):

Jimai ni kuingiza dhakari kwenye tupu ya mwanamke hata kama hukuteremsha manii. Mtu yeyote aliyefunga akifanya Jimai funga yake imebatilika, ni sawa funga ya faradhi au funga ya sunna.

Kisha kama amelifanya tendo hilo katika mchana wa Ramadhani hali ya kuwa yeye ni miongoni mwa wanao wajibika kufunga itamlazimu kulipa siku hiyo na kutoa Fidia ambayo ni kuacha huru mtumwa muislamu, akishindwa atafunga miezi miwili mfululizo na kama kuna siku amekula mchana (katika siku za fidia) bila ya udhuru wa kisheria (kama maradhi n.k) basi ataanza tena mwanzo, na akishindwa kufunga miezi miwili mfululizo atalisha masikini sitini na tumetangulia kutaja hapo kabla.

Hukumu hii itampata kila muislamu aliyefanya jambo hilo katika mchana wa Ramadhani ni sawa amemuingilia mwanamme au mwanamke, tupu ya mbele au nyuma, kwa halali au kwa zinaa, hata kama hajateremsha manii, na pia akimuingilia mnyama.

[12]- Surat Al-Baqara/187.

Jambo la Pili: Kujitoa manii kwa makusudi (kujichua):

Endapo mtu ametokwa na manii kwa kukumbatia, kupiga busu au kujichua kwa mkono au kwa sababu nyingine funga yake imebatilika kwa sababu hilo ni miongoni mwa matamanio ambayo ni wajibu kwa mfungaji kujiepusha nayo, kwa hadithi:

«يَتْرُكُ طَعَامَهُ وَشَرَابَهُ وَشَهْوَتَهُ مِنْ أَجْلِي»

"Anaacha chakula chake, kinywaji na matamanio yake kwa ajili yangu[13]".

- Lakini kama atabusu na kukumbatia bila kuteremsha manii funga ni sahihi na iliyo bora kwa vijana ni kujiepusha nalo.
- Ama kuteremsha manii kwa kuota ndoto (mchana wa Ramadhani) au kutafakari (mawazo mbaya) bila kubashiri kitendo jambo hilo halibatilishi Saumu, kwa sababu ndoto hutokea bila ya hiyari na kufikiria mtu amesamehewa kwa kauli ya Mtume swala na salamu zimshukie:

«إِنَّ اللَّهَ تَجَاوَزَ عَنْ أُمَّتِي مَا حَدَّثَتْ بِهِ أَنْفُسَهَا، مَا لَمْ تَعْمَلْ أَوْ تَتَكَلَّمْ»

"Allaah ameusamehe Umma wangu mambo wanayofikiria katika nafsi zao muda wa kuwa hawajafanya wala hawajasema[14]".

Jambo la Tatu: Kula na Kunywa:

Makusudio yake ni kufikisha chakula au kinywaji tumboni kupitia mdomo au pua. Ama kunusa manukato au harufu yoyote nzuri jambo hilo halifunguzi, kwa sababu hakuna hapo kitu kinachoingia tumboni.

---

[13]- Bukhari (1894).
[14]- Bukhari (5269).

Aina ya Nne: Kitu chochote kinachokaa nafasi ya chakula au kinywaji: nacho ni aina mbili:

1) Kuongezewa damu mtu aliyefunga jambo hili linafunguza.
2) Sindano za kuingiza vitamin C, hata kama si chakula lakini imekaa niaba yake.

- Ama sindano nyingine hazingii katika hukumu hii hata kama atapata ladha katika koo yake kwa sababu si chakula, maji wala hazikai niaba ya viwili hivyo.

Aina ya Tano: Kufanya Hijama (kuumika/kupiga chuku):

Hii ni aina tiba nzuri nayo ni kuitoa damu chafu mwilini kwa kutumia pembe, vikombe au Glass maalumu na Mtume swala na salamu zimshukie pia amesisitiza watu kufanya Hijama.

Jambo hili wanachuoni wametafautiana juu ya kufaa kwake kwa mtu aliyefunga, baadhi yao wanaona hadithi iliyokuja kukataza mtu kufanya Hijama hali ya kuwa amefunga imefutwa hukumu yake kwa hadithi nyingine zenye kuruhusu jambo hilo, na wengine wanaona kwamba mtu anafungua kwa kupiga chuku endapo atachoka na kudhoofika, kwa hiyo iliyo kuwa bora kwa mtu aliyefunga ni kujiepusha na jambo hilo.

Na kwa msimamo wa kwamba jambo hili linabatilisha funga itakuwa haifai kwa mfungaji kumtolea mtu mwingine damu isipokuwa ikilazimika kufanya hivyo na ikawa hakuna madhara yoyote kwa mfungaji na wakati huo atakuwa amefungua na atakuja kulipa siku hiyo. Ama kutokwa na damu za pua, vipele, majipu, kung'oa jino au kujichoma na kitu chenye ncha kali na mfano wake havibatilishi Saumu ya mtu, kwa sababu hakuna katika vitu hivyo athari yoyote kama ilivyokuwa katika Hijama.

Aina ya Sita: Kujitapisha:

Kujitapisha ni kukitoa chakula au maji yaliyo matumboni kupitia njia ya mdomo, na Mtume swala na salamu zimshukie amesema:

« مَنْ ذَرَعَهُ قَيْءٌ وَهُوَ صَائِمٌ فَلَيْسَ عَلَيْهِ قَضَاءٌ وَإِنِ اسْتَقَاءَ فَلْيَقْضِ »

"Yule ambaye yamemshinda yeye (hakuweza kuyazuia) matapishi hali ya kuwa amefunga (akatapika) hakuna juu yake kulipa, na aliye jitapisha alipe[15]".

Ni sawa amekusudia kwa kitendo kama kukamua tumbo lake n.k, au kwa kunusa kitu chenye kupelekea kutapika, au kwa kutazama kitu chenye kusababisha kutapika.

Aina ya saba: Kutoka damu ya Hedhi au Nifasi:

Mwanamke akiona damu ya Hedhi au Nifasi katika mchana wa Ramadhani funga yake imebatilika, sawa ni mwanzo wa mchana au jioni hata kama ni kitambo kidogo kabla ya kuzama jua.

Ndugu muislamu mambo hayo saba niliyo tangulia kuyataja ukiacha Hedhi na Nifasi hayabatilishi Saumu ya mtu isipokuwa kwa masharti matatu :

Sharti la Kwanza: Mtu awe anajua hukumu yake:

Kwa kauli ya Allaah:

﴿وَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ فِيمَا أَخْطَأْتُم بِهِۦ وَلَٰكِن مَّا تَعَمَّدَتْ قُلُوبُكُمْ ۚ وَكَانَ ٱللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا﴾

"Na hapana juu yenu lawama yoyote kwa mlivyokosea. Lakini ipo lawama katika yale ziliyo fanya nyoyo zenu kwa makusudi. Na Allaah ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu[16]".

---

[15]- Sunan Abi Daud (2382).

[16]- Surat Al-Ahzaab/5.

Ni sawa amefanya kwa kutojua hukumu yake kisheria mfano amedhania kwamba jambo hilo halibatilishi Saumu, au kwa kutojua hali au wakati kama vile mtu kudhania kwamba jua limezama akala au kudhania kwamba alfajiri bado akaendelea kula daku tahamaki akasikia watu wanaswali msikitini katika hali hizo zote haambiwi kwamba funga yake imebatilika.

Lakini akila kwa kudhani kwamba jua limezama kisha ukabainika kwake mchana basi atajizuia mpaka kuzama kwa jua na vivyo hivyo lau kama ameendelea kula kwa dhana ya kwamba bado alfajiri haijachomoza kisha akabainikiwa basi atajizuia mpaka jioni na funga yake ni sahihi wala hakuna kulipa.

Sharti la Pili: Awe anakumbuka:

Akifanya moja katika vitenguzi vya Saumu kwa kusahau funga yake haibatiliki, kwa hadithi:

«مَنْ نَسِيَ وَهُوَ صَائِمٌ فَأَكَلَ وَشَرِبَ، فَلْيُتِمَّ صَوْمَهُ، فَإِنَّمَا أَطْعَمَهُ اللَّهُ وَسَقَاهُ»

“Mwenye kusahau hali ya kuwa amefunga akala au akanywa akamilishe Saumu yake, hakika Allaah ndiye amemlisha na kumnywesha[17]”.

Kauli hii ya Mtume swala na salamu zimshukie kwamba akamilishe Saumu yake ni ushahidi juu ya usahihi wa Saumu yake, na pia kunasibisha kitendo chake cha kula na kunywa kwa Allaah ni ushahidi juu ya kwamba hakuna kosa lolote kwake. Lakini wakati wowote akikumbuka au kukumbushwa atajizuia na atatema kile kilicho mdomoni mwake kwa sababu hana tena udhuru, na mwenye kumuona mtu anakula hali ya kujua kwamba amefunga amkumbushe na huko ni kusaidieni katika wema.

[17]- Bukhari (1933) na Muslim (1155).

Sharti la Tatu: Afanye kwa hiyari yake (bila kulazimishwa):

Mtu akiyafanya hayo kwa kulazimishwa basi funga yake ni sahihi wala hakuna kulipa, kwa sababu Allaah ameondosha hukumu kwa mtu aliyekufuru kwa kulazimishwa na hali ya kuwa moyo umetulizana katika kumuamini Allaah pekee.

Ikiwa jambo hilo ni kwa mtu aliyekufuru basi aliye chini yake katika makosa ni jambo lenye kuwezekana In Shaa Allaah.

- Lau mtu amemlazimisha mke wake kufanya naye Jimai hali ya kuwa amefunga basi Saumu ya mkewe ni sahihi wala hatolipa, lakini naye akiridhia atalipa na pia atahusika na fidia mwezi wa Ramadhani, na kama ni funga ya sunna hakuna ubaya kwake kufungua na ajue kwamba mwanamke hatakiwi kufunga sunna isipokuwa kwa idhini ya mume.
- Lau kama limeingia vumbi tumboni kupitia mdomoni au ametawadha akatia maji mdomoni yakapitiliza mpaka tumboni bila kukusudia funga yake ni sahihi wala hatolipa.
- Pia haibatiliki funga kwa kutia wanja au dawa machoni au masikioni hata kama atahisi ladha kwenye koo yake.
- Wala haibatiliki funga kwa kuonja chakula endapo hakumeza wala kwa kunusa harufu ya Udi lakini asivute moshi wake puani ili asije kufungua kwa sababu kuna chembechembe zinapanda na moshi huenda zikapenya na kuingia tumboni.
- Wala haibatiliki Saumu kwa kupiga mswaki bali ni sunna kupiga mswaki wakati wa asubuhi mpaka jioni kwa mfungaji na asiye kuwa mfungaji lakini kwa mfungaji asitumie dawa.
- Inafaa kwa mtu aliyefunga kutumia kitu kwa ajili ya kupoza joto mwilini mwake kama vile kujimwagia maji baridi kichwani mwake.

Tanbihi: Ndugu muislamu jitahidi kuisoma dini yeko na kuifanyia kazi kwa sababu kuna mambo mengi yenye kuwatatiza watu wengi hasa katika zama zetu kwani wasemaji ni wengi hata ambao hawajulikani katika vikao vya elimu na hii ni natija ya kuenea kwa ujinga kiasi mtu hawezi kutafautisha kati ya uwongo na ukweli.

Isitoshe ni kawaida leo kumpata muislamu hajui kabisa kusoma Qur'an kitabu ambacho ukisoma herufi moja unapata thawabu kumi, kadhalika swala, na kundi kubwa la wanaoswali wanakosea kwa ksababu hawajui namna ya swala ya Mtume swala na salamu zimshukie. Na ndiyo maana waislamu wengi hustaajabu mafunzo sahihi ya dini yao na kumchukia msemaji wake kwa hoja hati amekuja na jambo jipya hawakuwa wamelisikia hapo kabla, hawajui masikini kuwa elimu ni kwa kusoma! Allaah anasema: **"Na wanao fanya juhudi kwa ajili yetu, Sisi tutawaongoza kwenye njia zetu[18]".**

Amesema Imam Tabariy Allaah amarehemu: **"Tutawaafikisha kupatia njia iliyonyooka, nako ni kupatia katika dini ya Allaah ambayo ni uislamu ambao Allaah amemtuma nao Muhammad swala na salamu zimshukie".** hivi kuna neema kubwa kama mtu kuongozwa njia iliyonyooka, ambayo unaiomba kila siku mara 17 ndani ya swala yako?! Usibabaishwe na maneno ya watu waliopatwa na pepesi za Shetani na kuchafuliwa akili zao wanaodhani kwamba mtu kusoma Dini yake ni sababu ya kuwa maskini, hizo ni fikra potofu: **"Shetani atakutieni khofu ya ufakiri na anakuamrisheni mambo machafu[19]".** Wallaahu a'alam.

Jumapili 10/ramadhani/1441h-3/5/2020m.

[18]- Surat Al-Ankabuut/69.
[19]- Surat Al-Baqara/168.